*Mulika, Na. 43 (1), 155-174*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Sauti za Usimulizi Zilivyotumika Kutoa Mtazamo wa Kisiasa katika Hadithi Fupi Teule

*Jenifer Desdely Chapanga*[1]
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
na
*Anna Nicholaus Kyamba*[2]
Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na43t1.9

**Ikisiri**

Mtazamo ni miongoni mwa vipengele vya usimulizi katika kazi za fasihi. Wahakiki, wachambuzi na watafiti wa kazi za fasihi wamejadili mtazamo kama kipengele cha fasihi kwa namna mbalimbali. Baadhi yao ni: Ferguson (1982), Monolov (2007) na Yirsaw (2016). Ferguson (1982) na Monolov (2007) wanadai kuwa kutokana na ubanifu wa hadithi fupi, mtazamo hasa wa wahusika hauelezwi bayana kutokana na matumizi ya nafsi ya kwanza au nafsi ya tatu. Naye Yirsaw (2016) anaeleza kuwa mtazamo katika usimulizi wa hadithi fupi uko bayana kupitia msimulizi. Mawazo ya wataalamu hawa yanakinzana. Hata hivyo, katika uhakiki wao waligusia kipengele cha mtazamo kiujumla pasi na kuhusisha masuala ya kisiasa, kijamii na kiuchumi, masuala ambayo yanahusishwa na mtazamo katika kazi za fasihi. Kutokana na hali hiyo, makala haya yanakusudia kuchunguza mtazamo kwa kujiegemeza katika nyanja mahususi. Hivyo, makala haya yamekusudia kuchambua sauti za usimulizi zilivyotumika kutoa mtazamo wa kisiasa katika hadithi fupi ya Shingo ya Mbunge ya Wamitila (2007) na Msomi Aliyebinafsishwa ya Nyangwine (2007). Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Naratolojia ambayo imetupatia kile ambacho Bal (1997) anakiita "zana" ili kutusaidia kubaini na kufafanua sauti za usimulizi zilizotumika kutoa mtazamo wa kisiasa katika hadithi fupi za Shingo ya Mbunge na Msomi Aliyebinafsishwa.

## 1.0 Utangulizi

Mtazamo ni kipengele kimojawapo cha usimulizi ambacho kimechunguzwa na wataalamu mbalimbali kama vile Msokile (1992), Wamitila (2003) na Rasley (2008). Msokile (1992) anaeleza kuwa mtazamo ni jinsi ya kuona mambo katika maisha na kuwa kila mtu ana namna ya kuyatazama mambo yanayomzunguka. Pia, anadai kuwa maudhui ya kazi za fasihi lazima yahusishe dhamira zinazotolewa na mtazamo. Naye Wamitila (2003) anaeleza kuwa mtazamo hutumiwa kuelezea jinsi msimulizi anavyoitazama hadithi yake pamoja na mahali anakoielekezea hadithi hiyo. Kadhalika, Rasley (2008) anaeleza kuwa katika usimulizi, sauti ndiyo chanzo

[1] **Baruapepe:** jeniferchapanga@gmail.com
[2] **Baruapepe:** annanicholausk@gmail.com

cha kupata mtazamo kwani kupitia sauti hizo, tunaweza kubaini hisia, msimamo na mawazo ambayo husaidia kueleweka kwa simulizi husika. Kadhalika, Fludernik (2009) na Kuhn (2009) wanajadili uhusiano wa mtazamo na utazamishaji kwamba ni mambo yasiyoweza kutenganishwa. Wataalamu hao wanaeleza kuwa ili mtazamo udhihirike, lazima kuwe na utazamishaji kulingana na nafasi aliyonayo msimulizi. Aidha, wanaeleza kuwa tunapata mtazamo kupitia utazamishwaji kutoka kwa mhusika au msimulizi. Kwa hiyo, kupitia utazamishwaji ndipo tunaweza kupata mtazamo wa mhusika au msimulizi. Hata hivyo, Kuhn (2009) anaeleza kuwa kuna ugumu wa kubainisha mtazamo katika usimulizi kama vile kuonesha: Nani anaongea? Wapi? Anafahamu nini kuhusiana na tukio? Ana mtazamo gani? Mtaalamu huyu anaeleza kuwa ugumu huo unatokana na mambo hayo kubadilika kila mara katika simulizi.

Wataalamu mbalimbali wamejadili kuhusu mtazamo katika usimulizi wa hadithi fupi. Wapo wataalamu wanaoona kuwa mtazamo katika usimulizi wa hadithi fupi haupo bayana. Kwa kuongozwa na fikra hizo, Ferguson (1982) na Monolov (2007) wanadai kuwa kutokana na ubanifu wa hadithi fupi, mtazamo, hasa wa wahusika, hauelezwi bayana kwa kuwa kuna matumizi ya nafsi ya kwanza au nafsi ya tatu. Kwa upande mwingine, Yirsaw (2016) anaona kuwa mtazamo katika usimulizi wa hadithi fupi uko bayana kupitia msimulizi ambaye ndiye anasimulia matukio ya wahusika. Hivyo, tunafahamu mtazamo na mawazo ya wahusika kupitia kwa msimulizi. Ijapokuwa wataalamu hao wameeleza mawazo yao kuhusu mtazamo katika hadithi fupi, mawazo yao yametofautiana kimtazamo. Tafiti zao zinaonesha kuwa mitazamo ipo katika hadithi fupi lakini kuna utata katika kubainika kwake katika usimulizi wa kazi mbalimbali. Hata hivyo, katika uchambuzi wa kazi za fasihi hasa kipengele cha mtazamo ni muhimu kuzingatia yanayozungumzwa katika kazi hizo kwa kuangazia nyanja za siasa, uchumi na jamii. Kwa kuwa utanzu wa hadithi fupi haujaangaziwa kikamilifu kama ilivyobainika katika tafiti za awali, makala haya yamekusudia kushughulikia utanzu huu ili kuchunguza namna sauti za usimulizi zilivyotumika kutoa mtazamo wa kisiasa. Hivyo, kwa kutumia Nadharia ya Naratolojia, makala haya yamechunguza ujitokezaji wa mtazamo wa kisiasa katika usimulizi wa hadithi fupi za *Shingo ya Mbunge* na *Msomi Aliyebinafsishwa.*

## 2.0 Nadharia ya Naratolojia

Naratolojia ni nadharia inayochunguza usimulizi unaopatikana katika matini. Matini hiyo inaweza kuwa imeandikwa, ya mdomo, imechorwa au imefinyangwa (Bal, 1997). Dhana ya naratolojia iliasisiwa na Tzvetan Todorov katika karne ya ishirini, ambapo mtaalamu huyo alichunguza ruwaza pana ya usimulizi iliyotawala hadithi zote (Keen, 2003). Keen (2003) anaeleza kuwa Nadharia ya Naratolojia imewashughulisha wataalamu wengi kabla ya karne ya ishirini kama vile Plato na Aristotle. Pia, anaeleza kwamba simulizi/hadithi inapaswa kuwa na sehemu tatu ambazo ni mwanzo, kati na mwisho zinazohusishwa na dhana ya mimesia na diagesia. Mtaalamu mwingine ni Vladimir Propp ambaye aliathiriwa na Umuundo

na aliiendeleza katika kuweka misingi ya uchunguzi wa kimofolojia wa dhana ya msuko wa hadithi (Prince, 1982; Wamitila, 2002; Rasley, 2008; Fludernik, 2009). Mathalani, Prince (1982) anaeleza kuwa usimulizi unahusu muundo wa simulizi ambao huweza kuwa katika matini yoyote. Prince anafafanua zaidi kuwa hadithi au habari inaweza ikasimuliwa kwa namna tofauti na watu mbalimbali; namna hizo hutofautiana na matini halisi. Naye Genette (1980) anaeleza kuwa nadharia hii ina misingi mitatu ambayo ni usimulizi, hadithi na ploti. Genette (1980) anaendelea kusema kuwa katika usimulizi ni muhimu tufahamu ni nani anayesimulia hadithi, yaani sauti inayosikika ni ya nani. Kimsingi, sauti hizo zimegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: sauti ya nafsi ya kwanza, ya pili, na ya tatu. Nafsi ya kwanza na ya pili hufungamanishwa na mwandishi wakati nafsi ya tatu, mara nyingi, huwa nje ya simulizi na haifungamani na nafsi ya mwandishi. Aidha, Genette (1980) anafafanua kuwa kuna uhusiano baina ya sauti na aina ya mtazamo, kwamba msimulizi na mtazamo ni vitu vinavyohusiana. Genette anaeleza kuwa msimulizi anaweza asihusiane na tukio bali mhusika. Pia, mtazamo unaweza kuwa wazi au usiwe wazi kutegemeana na nani anasimulia na kwa namna gani.

Bal (1997) anaeleza kuwa mwandishi humtengeneza msimulizi katika kazi yake akiwa na maana kuwa si mwandishi anayesimulia bali msimulizi. Nafasi ya msimulizi inaweza kuchukuliwa na mhusika anayehusika na tukio au msimulizi mwingine ambaye hahusiki na tukio. Bal (1997) anabainisha kuwa msimulizi anaweza kuwa katika nafsi ya kwanza, ya pili, au ya tatu; wakati mwingine nafsi zote huweza kusimulia na kutoa mtazamo fulani. Aidha, anaeleza kuwa suala la mtazamo linalowasilishwa katika tukio lina uhusiano baina ya mhusika, msimulizi na utazamishwaji. Naye Wamitila (2002), anaeleza kuwa katika Nadharia ya Naratolojia kuna mtazamo wa msimulizi au mwandishi, mtazamo unaohusu masuala fulani ambayo humtazamisha msomaji au mtazamaji. Hivyo, tutafahamu ni nani, nini kinazungumzwa na mtazamo gani unaotolewa kuhusiana na kile kinachozungumzwa. Kwa kutumia Nadharia ya Naratolojia, makala haya yametumia mawazo ya Genette (1980), Bal (1997) na Wamitila (2002) katika kuchunguza namna sauti za usimulizi zinavyotoa mtazamo wa kisiasa katika hadithi fupi za *Shingo ya Mbunge* na *Msomi Aliyebinafsishwa.*

## 3.0 Mbinu za Utafiti

Makala haya yanatokana na sampuli wakilishi ya hadithi fupi mbili (2) za Kiswahili ambazo ziliteuliwa miongoni mwa hadithi fupi 10 zilizosomwa kutoka katika diwani ya *Shingo ya Mbunge na Hadithi Nyingine* (2007). Kupata hadithi fupi teule, usampulishaji lengwa ulitumika kuteua hadithi fupi mbili (2) zinazosawiri mtazamo wa kisiasa. Mbinu iliyotumika kukusanya data ni ya usomaji makini wa matini teule. Mbinu hii ilihusu upitiaji wa matini teule kwa makini ili kupata data za msingi zinazohusiana na mada hii. Hivyo, mbinu hii ilitumika kusoma hadithi fupi ya *Shingo ya Mbunge* (2007) na *Msomi Aliyebinafsishwa* (2007) na kufanyiwa

uchambuzi kulingana na malengo ya makala haya. Aidha, kupitia mbinu hii sauti zilizotumika kuonesha mtazamo wa kisiasa zilibainishwa.

## 4.0 Muhtasari wa Hadithi Fupi Teule

Makala haya yametumia hadithi fupi teule mbili ambazo ni *Shingo ya Mbunge* (Wamitila, 2007) na *Msomi Aliyebinafsishwa* (Nyangwine, 2007). Muhtasari wa hadithi hizo ni kama ifuatavyo:

### 4.1 *Shingo ya Mbunge*

Hadithi ya *Shingo ya Mbunge* inapatikana katika kitabu cha hadithi fupi kiitwacho *Shingo ya Mbunge na Hadithi Nyingine* (2007). Kitabu hicho kimehaririwa na K.W. Wamitila na kuchapishwa na Vide ~ Muwa (2007). Hadithi hii inahusu wanakijiji wa Mwengea na mbunge wao Mheshimiwa Dan Magraba. Wananchi wa Mwengea wanatamani sana kupata mbunge kutoka katika tarafa ya Mwengea. Katika kipindi cha uchaguzi, kampeni zinafanyika na wananchi wanahakikisha wanampigia kura mgombea ubunge anayetoka tarafa yao. Wananchi wanamchagua Dan Magraba kuwa mbunge wa eneo la Mwengea. Wakati huo wanamwita kishingo kwa sababu shingo yake ni ndefu na nyembamba. Dan Magraba anapenda kujilinganisha na twiga kwa kuwa ana shingo ndefu, hivyo, anaamini kuwa ana uwezo wa kuona mbali. Wananchi hao wana matumaini makubwa kwa Dan Magraba; wanaamini kuwa atawaletea maendeleo. Baada ya uchaguzi, mbunge anabadilika na kuwasaliti kwa kijilimbikizia mali na kuishi maisha ya kifahari. Wakati huu shingo yake inabadilika kuwa nene kutokana na kunawiri. Kutokana na hali hiyo, Wanamwengea wanaamua kumfuata nyumbani kwake lakini anawapuuzia, anawaacha hapo na kuondoka kwenda katika shamba la kahawa. Wananchi hao wanaona tu shingo ya mbunge. Wananchi wanaamua kurudi kijijini baada ya kutofanikiwa kuonana naye.

### 4.2 *Msomi Aliyebinafsishwa*

*Msomi Aliyebinafsishwa* ni hadithi fupi ambayo inapatikana pia kitabu cha hadithi fupi kiitwacho *Shingo ya Mbunge na Hadithi Nyingine* (2007) iliyohaririwa na K. W. Wamitila na kuchapishwa na Vide~Muwa. Hii ni hadithi inayohusu familia ya Mama Msagane na wanakijiji wa Kong’amu. Mama Msagane anabahatika kupata watoto pacha, mmoja anaitwa Nyaguchiro na mwingine Entakana. Watoto hao wanapelekwa shuleni lakini baada ya mama yao kufariki, Entakana anashindwa kuendelea na masomo, hivyo, anaamua kujiunga na jeshi la kujenga nchi. Nyaguchiro anaendelea na masomo kwa sababu anasomeshwa na wanakijiji ambao wana matumaini makubwa kwake. Hatimaye, Nyagichuro anahitimu ngazi ya uzamivu (PhD) katika kozi ya Sera na Ubinafsishaji na kupewa cheo kuwa Mkurugenzi wa Ubinafsishaji katika taifa. Hata hivyo, Nyaguchiro anaanza kutumia madaraka ya kisiasa kwa ubinafsi kwa kufanya anavyotaka. Pia, anawasaliti wanakijiji wa Kong’amu kwa kuwabinafsisha wao na rasilimali zao kwa

mwekezaji. Hivyo, kupitia hadithi hizi teule, sauti za usimulizi zilizotumika kutoa mtazamo wa kisiasa zimebainika.

## 5.0 Sauti za Usimulizi na Mtazamo wa Kisiasa katika Usimulizi wa Hadithi Fupi Teule

Sauti za usimulizi ni zile zinazotumika kuelezea matukio katika hadithi. Sauti hizi ni muhimu katika usimulizi wa hadithi kwa sababu hutuwezesha kufahamu nani anayesimulia. Kupitia sauti ya anayesimulia, tunaweza kufahamu mengi kuhusu mtazamo wa jambo linaloongelewa kwa kuwa sauti hiyo hutupatia hisia na mitazamo mbalimbali. Hii inamaanisha kuwa mtazamo unachambuliwa kulingana na namna wahusika wanavyoyaona mambo katika hadithi kwa kuwa wahusika ndio hupewa majukumu ya kuwasilisha jambo hilo. Hivyo, msimulizi au mhusika anaweza kutoa mawazo yake kwa namna anavyoona yeye kulingana na uhusiano wake na tukio husika. Kama asemavyo Rimmon-Kenan (2002), usimulizi wa hadithi unapaswa kupangwa kulingana na matukio, wakati, tabia na mazingira ya wasomaji wa hadithi husika. Uhusiano wa tukio, wakati, tabia ya mhusika au msimulizi unaonekana kupitia sauti za usimulizi ambazo hutumika kutoa mtazamo. Hadithi husimuliwa kwa nafsi mbalimbali kupitia msimulizi ambaye hutumia sauti za nafsi hizo kutoa mitazamo[3] mbalimbali inayojitokeza ndani ya matini teule. Hivyo, katika makala haya tumechambua sauti zilizotumika kutoa mtazamo wa kisiasa kwa kuangalia sauti ya mwenye mtazamo husika. Sauti hiyo huweza kuwa ya mhusika, msimulizi au mtu yeyote katika hadithi. Sauti hiyo ipo katika makundi matatu ambayo ni ‘mimi’, ‘wewe’ au ‘yeye’ ambazo zimegawanywa katika nafsi ya kwanza, nafsi ya pili na nafsi ya tatu.

### 5.1 Sauti ya Nafsi ya Kwanza

Sauti ya nafsi ya kwanza huwakilishwa na mofu “ni” katika umoja na mofu “tu” katika wingi. Aidha, kupitia nafsi ya kwanza tunaweza kumbaini mhusika mwingine ambaye ana uhusiano na msimulizi wa nafsi ya kwanza. Uhusiano huo ni kama vile mimi-yule, yule-mimi**.** Katika uhusiano huo, msimulizi anasimulia kwa mtazamo wake mwenyewe na kupitia msimulizi wa nafsi ya kwanza tunabaini wahusika wengine. Kwa ujumla, sauti ya nafsi ya kwanza iliyojitokeza katika hadithi fupi ya *Shingo ya Mbunge* na *Msomi Aliyebinafsishwa* ipo katika makundi kadhaa ambayo ni: msimulizi anayesimulia maisha yake yanayomhusu, msimulizi kama shahidi, na msimulizi wa nafsi ya kwanza anayesimulia kuhusu wahusika wengine. Usimulizi wa sauti ya nafsi ya kwanza umejitokeza katika hadithi fupi ya *Shingo ya Mbunge* ambapo mhusika msimulizi anatumia umoja na wingi katika simulizi kutoa mtazamo wa kisiasa. Msimulizi anasimulia hali mbaya ya mifugo

[3] Ikumbukwe kuwa katika usimulizi, mwandishi hasimulii hadithi bali msimulizi ambaye sauti yake inasikika kupitia nafsi tofauti. Hivyo, kunaweza kuwa na sauti mbalimbali za wahusika ambazo zinatoa mawazo na misimamo. Kwa hiyo, mitazamo ya kisiasa inayotolewa ni mingi kulingana na nafsi hizo. Mitazamo hiyo inaweza kukubaliana au kutokukubaliana na jambo la kisiasa linaloongelewa.

iliyokuwapo katika jamii yao ambayo imesababishwa na ukame ulioleta athari kwa wananchi. Msimulizi anatoa mtazamo wake ambao unamhusisha mbunge anayetakiwa kuwasikiliza wananchi wake ili kunusuru hali hiyo. Hilo linadhihirika katika lifuatalo ambapo msimulizi anasema:

> "Ng'ombe wetu waliendelea kupukutika kama mkuyu labda mara hii atasikiliza kilio cha watu waliomchagua" **niliwaza** (uk. 48).

Katika dondoo hilo hapo juu, msimulizi ambaye ni mwananchi wa kawaida anatoa mtazamo wake wa kisiasa wa kutowajibika kwa viongozi kutokana na mawazo yake kwa kuwa anahusika moja kwa moja na adha iliyopo. Msimulizi ambaye pia ni mwananchi, anatamani madai yao yasikilizwe na mbunge ambaye walimchagua na hatimaye awatatulie changamoto zao. Kimsingi, msimulizi anapotoa maoni yake kuhusu jambo fulani, huwa anaonesha uhusiano wake na anachokizungumzia. Kutokana na uhusiano huo, msimulizi anaonesha mazingira ya kisiasa yaliyomo katika jamii yao; mazingira ya kiongozi kutokuwa karibu na wananchi wake. Hali hii imemwathiri sana msimulizi kiasi cha kueleza mawazo yake kulingana na athari hiyo. Msimulizi wa nafsi ya kwanza anapotoa mtazamo, mara nyingi huonesha uhusiano wake na anachokizungumzia katika hadithi hiyo (Prince, 1982). Hii inamaanisha kuwa msimulizi anaonesha yupo karibu na simulizi, yaani ni mhanga wa jambo hilo. Aidha, ni wazi kuwa katika sauti ya nafsi ya kwanza kuna uhalisia fulani wa maisha ya msimulizi kwa kuwa ndiye anayesimulia.

Sambamba na hilo, msimulizi anaonesha mtazamo wa umoja kwa sauti ya nafsi ya kwanza inayodhihirishwa na mofu "ni" na "tu" kwa wakati mmoja. Kupitia sauti ya nafsi ya kwanza, msimulizi anaonesha namna walivyopata wazo la kumfuata mbunge nyumbani kwake na kumweleza shida zao. Katika tukio hili msimulizi mhusika anasema:

> **Nilikumbuka** jinsi wanakijiji walivyokuwa wametuchagua **niliyakumbuka hata maneno ya siku hiyo** "kumbukeni ni muhimu muwe pamoja, muwe kitu kimoja. Hakikisheni kuwa anapata picha ya umoja wetu, umoja wetu, nia zetu. Lazima **tuiokoe** jamii yetu… **tulipaswa** kusafiri pamoja (uk. 47).

Katika dondoo hilo, sauti ya msimulizi imetumika kutoa mtazamo wa kisiasa wa kutowajibika kwa viongozi. Msimulizi anasimulia namna wanakijiji wanavyowatuma kwenda kwa mbunge ili kupata suluhisho la changamoto zao. Kwa kufanya hivyo, msimulizi anakumbuka maagizo ya wananchi wengine kuhusu mbunge wao. Kupitia mtazamo huo, tunaona namna wananchi walivyo na umoja kwa hatua waliyochukua baada ya kuona kuwa hakuna anachokifanya mbunge wao kwa ajili ya maendeleo katika kijiji chao. Aidha, katika dondoo hilo tunaona sauti

ya msimulizi ni mhusika ambaye anawatetea wananchi kwa kuwa ametumia kiambishi "ni" na "tu". Hapa inaonesha kuwa sauti ya msimulizi ni ya mhusika ambaye ni sehemu ya hayo ayasemayo. Hata hivyo, anasimulia kwa mtazamo wake kwa sababu ndiye anayesimulia kuhusu matukio ya hadithi. Kwa mujibu wa Bal (1997), sauti inayosimulia kwa kutumia nafsi ya kwanza ikifuatiliwa kwa jicho la uhusika unaweza kukubaliana na mtazamo wa nafsi hiyo. Kwa hiyo, tunaona kuwa mtazamo wa umoja, mshikamano na ushirikiano wa wananchi kupitia sauti ya nafsi ya kwanza katika hali halisi unakubalika ili kufanikisha jambo fulani.

Kadhalika, katika hadithi ya *Shingo ya Mbunge*, kuna sauti ya nafsi ya kwanza ambayo imejitokeza kupitia msimulizi anayedhihirisha mtazamo wake kuhusiana na utajiri wa Dan Magraba baada ya kuwa mbunge. Msimulizi mhusika anasema:

> "**Niligeuka** na kuangalia lile jengo lililokuwa limemmeza Mbunge kama tumbo la chatu... Lazima hivi ndivyo inavyokuwa baada ya mtu kuwa Mbunge" **nilijiambia** (uk. 54).

Kupitia nukuu hiyo, msimulizi anaonesha mtazamo wake kwa kutumia sauti ya nafsi ya kwanza kueleza kama shahidi wa jambo hilo, kuwa ubunge, ambayo ni nafasi ya kisiasa, ni chanzo cha utajiri. Kwa hiyo, kulingana na mazingira hayo ya kisiasa, tunaalikwa kusikia namna ambavyo mbunge wa Mwengea ametumia fursa hiyo kujitajirisha na kujinufaisha mwenyewe pasi na kuwasaidia wananchi wake. Hapa msimulizi anatoa mtazamo wa kisiasa unaodhihirisha ufisadi wa viongozi mara tu wapatapo nafasi za kuwaongoza wananchi. Kwamba, viongozi wengi wanajali masilahi yao binafsi. Jambo hili linatokana na mbunge kujenga nyumba ya kifahari kupitia ubunge wake huku akiwaacha wananchi katika adha mbalimbali. Suala hili linadokeza kwamba viongozi hawawajali wananchi, wanachoangalia ni masilahi yao binafsi mara tu wapatapo uongozi. Aidha, katika nukuu hiyo, kupitia nafsi ya kwanza, msimulizi anatoa mawazo au maoni ya jambo analoliona kwa uhuru kulingana na ufahamu na hisia zake kama asemavyo Burkhard (2009) kuwa kwa mtazamo wa sauti ya nafsi ya kwanza, mhusika msimulizi anakuwa huru kueleza mawazo yake kuhusu jambo fulani, ambapo mawazo hayo huwa ya moja kwa moja.

Pia, msimulizi ametumia nafsi ya kwanza kusimulia mtazamo wa kisiasa kuhusu uchaguzi wa viongozi wa kisiasa katika hadithi fupi ya *Shingo ya Mbunge.* Suala hili linaonekana kwa wahusika Sota na Levina ambao wanatofautiana mitazamo. Jambo hili linajitokeza kipindi cha uchaguzi wa viongozi wa kisiasa ambapo wananchi wa Mwengea wanatakiwa kupiga kura ili kumchagua mbunge. Katika kipindi cha uchaguzi, mhusika Sota (mumewe Levina) hakuruhusu mtu yeyote katika familia yake akamchague kiongozi kwa kuwa hakupata gawio la fedha kutoka kwa mgombea (uk. 46). Mkewe Levina alionesha mtazamo wake wa kisiasa

kupitia sauti ya nafsi ya kwanza kuwa ni haki yake ya msingi ya kumchagua kiongozi anayemtaka. Levina anaeleza hayo katika dondoo lifuatalo:

> ‘‘**Mimi** lazima **nipige** kura, lazima **nitumie** haki na uwezo wangu kuamua nani atakwenda **kutuwakilisha** bungeni” (uk. 47).

Kwa hiyo, kupitia Dondoo Na. 4 hapo juu tunaona kuwa sauti ya mwananchi katika nafsi ya kwanza inabainisha mitazamo ya kidemokrasia katika masuala ya uchaguzi wa viongozi wa kisiasa. Mtazamo wa Levina ni wa kupigania haki yake wakati mtazamo wa Sota unalenga kupoteza na kujidhulumu haki ya kupiga kura kumchagua kiongozi kwa sababu hakupata gawio la fedha kutoka kwa wagombea ubunge. Kupitia sauti ya nafsi hii, unajengwa mtazamo kuwa uchaguzi wa viongozi hugubikwa na rushwa kwa upande mmoja, na kwa upande mwingine, unajengwa mtazamo wa kutumia haki ya kidemokrasia katika kuchagua viongozi.

Vilevile, katika hadithi fupi ya *Shingo ya Mbunge* sauti ya nafsi ya kwanza imetumika kuhamasisha wananchi kushiriki katika kampeni ya uchaguzi wa viongozi wa kisiasa ili kupata kiongozi atakayewawakilisha bungeni. Sauti hiyo inadokeza mitazamo ya wahusika, Faustine na Dan Magraba, mbunge, baada ya shughuli ya uchaguzi. Msimulizi kupitia Faustine anasema:

> “Natumaini damu hii itayatakasa maovu yetu… alipaza sauti Faustine. Oh, Faustine milele **nitathamini** sadaka hii” alisema Dan Magraba (uk.48).

Katika nukuu hiyo, mhusika Faustine anaonesha mtazamo wake baada ya kumpata mbunge, Dan Magraba, aliyeshinda kwa kura nyingi. Wananchi wanaonesha furaha yao baada ya kupatikana kwa mbunge ambaye atawawakilisha. Mtazamo wa Faustine kwa Dan Magraba, unaonesha kuwa wananchi wana matumaini na matarajio makubwa kwa kiongozi wao. Naye mbunge mwanzoni anaonesha nia ya kuwasaidia wananchi wake. Katika tukio hilo la kujitoa mhanga katika uchaguzi wa kiongozi, tunaona kuwa wahusika hao wana mitazamo inayoendana ambapo wametoa mitazamo yao kulingana na hisia zao na ufahamu wao. Kwa mujibu wa Nadharia ya Naratolojia, mitazamo inayotolewa na wahusika mbalimbali kuhusu tukio au jambo moja mara nyingi hutolewa kwa kufuata hisia na ufahamu wa wahusika hao (Wamitila, 2008). Kupitia sauti hii, tunapata mtazamo wa matumaini ya wananchi na ukombozi wa wanajamii kupitia kiongozi wao.

Kadhalika, katika hadithi fupi ya *Msomi Aliyebinafsishwa* sauti ya nafsi ya kwanza imetumika kutoa mtazamo wa kisiasa. Nyagichuro anasema:

> ...**mimi** ni msomi wa nchi. **Sina** muda mwingi wa kupoteza. **Nina majukumu** mengi yanayonisubiri. Kwanza, bwana Mkubwa wa Ikulu ananisubiri. Hivyo **naomba nianze** na pointi zangu moja kwa moja (uk 10).

Katika dondoo hili tunapata mtazamo wa uongozi mbaya kupitia sauti ya nafsi ya kwanza. Mtazamo huo anautoa mbunge kulingana na nafasi aliyo nayo ya usomi ambapo anaeleza majukumu yanayomkabili na namna ambavyo hana muda wa kuongea na wananchi. Kauli hizo za mbunge zinaonesha uongozi mbaya wa viongozi wa nchi mara tu wapatapo nafasi za uongozi.

Pia, kuna sauti ya nafsi ya kwanza ya autodaijetiki[4] (*autodiegetic*) katika nafsi ya kwanza ambayo imejitokeza katika hadithi ya *Shingo ya Mbunge*. Fludernik (2009) anaeleza kuwa katika usimulizi wa aina hii msimulizi wa nafsi ya kwanza anatoa maoni na mawazo ya wahusika wengine. Lengo la usimulizi huu ni kuonesha sauti za wahusika wengine katika simulizi. Usimulizi huu unatokana na ukweli kuwa msimulizi wa nafsi ya kwanza hawezi kujibana tu katika kuelezea maisha yake pekee bali lazima asimulie maisha ya wahusika wengine ambao wana uhusiano naye katika kukamilisha tukio husika.

Katika hadithi fupi ya *Shingo ya Mbunge*, msimulizi ametumia sauti ya autodaijetiki ya nafsi ya kwanza kusimulia kuhusu wahusika wengine. Usimulizi huu umejitokeza pale ambapo msimulizi anasimulia namna mbunge alivyojenga jumba la kifahari kupitia fedha za ubunge zinazotokana na ufisadi ilhali wananchi wanaishi katika hali ngumu. Msimulizi anaeleza katika dondoo linalofuata:

> “Amejenga bahari ya nyumba baada yake na wabunge wenzake kujilipa mamilioni ya fedha. Wanasema ana majumba mengi ajabu kwenye mitaa ya matajiri”. **Niliyakumbuka** maneno yaliyosemwa na kijana mmoja wa kijijini aliyeelekea kuyafahamu mambo mengi tuliyokuwa hatuyajui sisi (uk. 51).

Katika dondoo hilo hapo juu, sauti ya msimulizi inatoa mtazamo wa kisiasa kwa kutumia nafsi ya kwanza kuonesha masuala ya uhujumu uchumi kwa viongozi wa kisiasa. Aidha, kutokana na mazingira hayo ya mbunge kutumia ubunge kujinufaisha mwenyewe, msimulizi anaonekana kutokukubaliana na jambo hilo. Msimulizi anatueleza kuhusu matabaka katika jamii kwa kuonesha utofauti wa hali ya maisha baina ya viongozi wa kisiasa na wananchi wa kawaida. Kwa hiyo, katika usimulizi wa autodaijetiki msimulizi anatazama kwa nje ili kuonesha maisha ya wahusika wengine katika simulizi.

[4] Usimulizi wa autodaijetiki ni ule ambao msimulizi anatazama matukio na mawazo ya wahusika wengine kwa nje lakini yupo katika simulizi na wakati mwingine anaweza akubaliane au asikubaliane na mitazamo, fikra na mawazo ya wahusika hao.

Mfano mwingine wa usimulizi wa sauti ya nafsi ya kwanza ya autodaijetiki umejitokeza ambapo msimulizi anasimulia tukio la kampeni kwa wagombea na wananchi wao. Msimulizi anasema:

> Siku za kampeni walitokeza mmoja mmoja tu kuwanunulia watu ndizi, maembe na mpira, kwa vikundi vya michezo. Wanasema, "huu ni mwanzo tu; ngojeni mtaona mabadiliko makubwa **mkinichagua,**" waliahidi kila wakati. Watu nao kwa tamaa kubwa walimeza chambo hicho; wapiga kura nao wakapotea kabisa. "Hawa wakishakuwa wabunge ni basi; uso hauonekani ni shingo zao tu" (uk. 54)

Katika nukuu hiyo, msimulizi ni mhusika katika hadithi ambapo anaeleza matendo ya wahusika wengine. Mbali na sauti ya msimulizi kusikika kutoa mtazamo, sauti ya watu wengine inasikika katika mtazamo wa kisiasa. Hivyo, kupitia msimulizi tunaona mtazamo wa wahusika wengine ambao ni viongozi wa kisiasa wanavyotumia kampeni kwa udanganyifu, kutoa rushwa, usaliti na mambo mengine ambayo wananchi wanakutana nayo kipindi cha kampeni. Wananchi wanakutana na adha hizo kutokana na kutokuwa na uelewa wao. Japokuwa wananchi wenyewe wanawachagua viongozi hao, lakini wanabaki katika hali ngumu ya maisha kwani baada ya uchaguzi viongozi hao hawaonekani tena wala hizo zawadi wananchi hawazipati tena.

Kutokana na mjadala huu, tunaweza kusema kuwa msimulizi huweza kutumia usimulizi wa sauti ya nafsi ya kwanza tofautitofauti ili kuonesha mitazamo mbalimbali na kuwa na mawanda mapana kwa wahusika. Rasley (2008) anaeleza kuwa msimulizi hutumia sauti mbalimbali ili kuonesha mitazamo mbalimbali kwa namna tofauti na mitazamo hiyo huwa muhimu sana katika hadithi.

**5.2 Sauti ya Nafsi ya Pili**

Sauti hii hutumia kiambishi "wewe" au "u" katika umoja na "m" au "ninyi" katika wingi. Kwa kawaida, katika sauti hii mara nyingi msimulizi huwa analenga kumshirikisha msomaji katika simulizi. Fludernik (2009) anaeleza kuwa mwandishi hawezi kujifungia katika usimulizi wa nafsi ya kwanza na ya tatu pekee, kwani anahitaji kubadili usimulizi wake hasa anapokusudia kubadili mtazamo wake. Usimulizi unaotumia sauti ya nafsi ya pili, mara nyingi, msimulizi anazungumza na msomaji kwa kuwa anamwona. Msimulizi anaweza kuchukua jukumu la kuwasiliana na hadhira moja kwa moja ili kudumisha mahusiano kati yao katika simulizi (Wambui, 2018). Kulingana na mawazo ya wataalamu hawa, makala haya yamebaini kuwa mtazamo wa kisiasa umejitokeza katika sauti ya nafsi ya pili kwa namna mbili: mosi, sauti ya msimulizi inapozungumza na msomaji; pili, sauti za wahusika katika mazungumzo kama tuonavyo katika hadithi teule.

Katika hadithi fupi ya *Shingo ya Mbunge*, sauti ya nafsi ya pili inajitokeza msimulizi anapomshirikisha msomaji katika simulizi. Haya yanadhihirika pale msimulizi wa nafsi ya pili anapotoa mtazamo wake kuhusu tukio la uchaguzi, hususani namna mbunge alivyopatikana. Msimulizi anatueleza mtazamo wake ili wasomaji waone uaminifu wake kwa hatua walizochukua kukabiliana na hali waliyo nayo. Hilo linajidhihirisha katika Dondoo Na. 9 kama msimulizi anavyoeleza:

> Labda **unaweza** kuelewa kwa nini sote tulikuwa na matumaini makubwa, tulikuwa na ndoto…" (uk. 54).

Katika dondoo hilo hapo juu, msimulizi anatumia sauti ya nafsi ya pili ambayo inawakilishwa na kiambishi "u" akimaanisha wewe unayesoma ndiwe unashirikishwa mtazamo wake. Katika mtazamo huo wa kisiasa kuna jambo linazungumzwa na msimulizi ambalo anatushirikisha ili tuelewe hali wanayopitia wananchi kutokana na viongozi kutowajibika ipasavyo. Kwa hiyo, tunaweza kusema kuwa sauti ya nafsi ya pili katika simulizi huleta athari fulani kwa msomaji kwa sababu msimulizi anamshirikisha msomaji mawazo yake.

Aidha, katika hadithi ya *Shingo ya Mbunge*, sauti ya nafsi ya pili inajidhihirisha kupitia mazungumzo baina ya wahusika. Kupitia sauti ya nafsi ya pili, wahusika hao wanaeleza mtazamo wao kuhusu madaraka ya kisiasa na kutoa amri kwa watu wengine. Msimulizi anasema:

> Sina uwezo
> Lakini si **unaiwakilisha** serikali?
> Hilo najua
> Basi hupata amri!
> Kwani nasema nini
> **Unasema nini kwani?**
> Ni vigumu! Labda **mtaelewa** methali yetu bora. Kuna majabali
> ambako mijusi haipandi kuotea jua (uk.50)

Katika dondoo hilo, tunaona mazungumzo baina ya wahusika wakitumia sauti ya nafsi ya pili. Kupitia mazungumzo hayo tunaona mtazamo wa kisiasa kuhusu mamlaka ya viongozi. Chifu, mhusika mmojawapo, anaona kwamba hana mamlaka ya kutoa amri kwa watu, na kwamba kuna watu wenye mamlaka hayo ambao ni viongozi wakubwa ijapokuwa hata yeye anawakilisha serikali. Licha ya wahusika hao kuzungumza wenyewe, pia wanamfikirisha msomaji kutokana na jambo wanalozungumzia ili kutengeneza maana. Kwa mfano, mhusika Chifu anaposema:

> "Labda **mtaelewa** methali yetu bora. Kuna majabali ambako mijusi haipandi kuotea jua" (uk.50).

Mtazamo huo unaojitokeza katika dondoo hilo hapo juu hauwafikirishi wahusika pekee wanaozungumza bali pia msomaji. Matumizi ya sauti ya nafsi ya pili hulazimisha msomaji kushiriki kutengeneza maana ya simulizi (Chapanga, 2021). Kwa hiyo, msomaji pia hufikiri mawazo ya wahusika ili kutengeneza maana ya simulizi (Rasley, 2008). Kwa mfano, msomaji huweza kutafuta maana ya methali iliyo katika nukuu ili kuelewa kwa undani zaidi.

Katika hadithi ya *Msomi Aliyebinafsishwa*, sauti ya nafsi ya pili inajitokeza kupitia mhusika Mama Msagane anapozungumza na watoto wake, Nyagichuro na Entakana. Mama Msagane anazungumza kuhusu hatua ambazo hazina budi kuchukuliwa dhidi ya usaliti na udikteta kwa viongozi. Sauti ya nafsi ya pili inajitokeza katika maneno yanayozungumzwa na mhusika Mama Msagane akitoa maoni yake kama wosia kwa wanawe katika kupigania haki na kuitafuta demokrasia ya kweli. Mama Msagane anasema:

> …**msimame** *kidete* kuutangazia ulimwengu juu ya ukatili wa viongozi wa Kong'amu. **Ujulishe** ulimwengu juu ya udikteta wa viongozi wetu. Ijapo wataziba masikio. Ijapo watawatia vumbi machoni mwenu, lakini jaribuni kunena kwa ishara ili ujumbe huu wa USALITI ufike kila pande ya ulimwengu (uk. 3).

Hapa sauti ya mhusika mama Msagane inaonesha mtazamo wa kutoridhishwa na uongozi wa kong'amu. Sauti hiyo inahamasisha hadhira kupinga uongozi mbaya kutokana na viongozi kuwa wasaliti na madikteta. Kwa kutumia sauti ya usimulizi wa nafsi ya pili, tumeweza kubaini kuwa mhusika Mama Msagane ametumia nafsi ya pili kutoa mtazamo ambao unatetea masilahi kwa wananchi pamoja na haki ya kisiasa. Pia, sauti ya nafsi ya pili imetumika kuleta ukombozi wa jamii pamoja na demokrasia ya kweli kwa wananchi.

Kadhalika, katika hadithi ya *Msomi Aliyebinafsishwa* mhusika Mama Msagane anazungumza na wanawe, Entakana na Nyagichuro, kuhusu demokrasia ya kweli na haki ya maendeleo kwa wananchi wote kama inavyojitokeza katika linalofuata. Msimulizi anasema:

> Hizi zote ni dalili za wazi kuwa **mnahitaji** demokrasia ya kweli na wala si demoghasia. Kusikiliza maoni ya pande nyingine za dunia. Kuona mabadiliko ya ulimwengu. **Mnakiu** ya haki ya maendeleo… Yashikeni matumbo yenu huku mkisema: NJAA! NJAA! NJAA! YA HAKI YA MAENDELEO! Hii itadhihirisha waza kuwa hamridhiki na misaada mpewayo toka ng'ambo. **Mnatakiwa** kutupilia mbali uchumi tegemezi (kur. 3-4).

Kupitia dondoo hilo, tunaona kuwa sauti ya msimulizi inajaribu kutushirikisha mtazamo wake na hisia zake za kisiasa kuhusiana na demokrasia. Kwa hiyo, katika

nafsi ya pili licha ya msimulizi au mhusika kuzungumza na wahusika wengine; pia, anazungumza na msomaji kuwa ana nafasi katika hadithi hiyo. Kwa mantiki hii, msomaji katika sauti ya nafsi ya pili ni sehemu ya hadithi.

Si hivyo tu, pia katika hadithi fupi ya *Msomi Aliyebinafsishwa* sauti ya nafsi ya pili inajitokeza katika wimbo ambao ulitungwa kwa ajili ya kiongozi Nyagichuro. Wimbo huo ambao unaimbwa kwa sauti ya nafsi ya pili, unaonesha mtazamo wa kejeli na wa kumlaani kiongozi huyo kulingana na matendo yake ya ubinafsishaji na usaliti kwa Wanakong’amu. Katika dondoo lifuatalo msimulizi anasema:

> Nyagichuro mtoto wa Mama Msagane
> **Utafanya** nini Kong’amu?
> Akheri usingezaliwa
> **Umetuletea** balaa kubwa
> **Umekubali** kubinafsishwa
> Huku una akili timamu!
> **Umelaaniwa** ARDHINI
> **Umelaaniwa** MBINGUNI
> MIZIMU YOTE IMEKUBALI LAANA YAKO. (uk. 9)

Katika nukuu hapo juu, tunaona jinsi sauti ya nafsi ya pili ilivyojitokeza kwa wahusika wananchi wa Kong’amu ambao wanamwimbia kiongozi Nyagichuro. Msimulizi kupitia Wanakong’amu, anazungumza na Nyagichuro kupitia wimbo ambao unaonesha mtazamo wao wa kumlaani na kumkejeli Nyagichuro kutokana na ubinafsishaji alioufanya kijijini hapo. Kutokana na nukuu hiyo, tunaweza kusema kuwa msimulizi anapotumia sauti ya nafsi ya pili anaonesha uhusiano wake na simulizi. Kuna uhusiano baina ya msimulizi wa sauti ya nafsi ya pili na simulizi au hadithi kwa sababu msimulizi ni miongoni mwa wahusika wanaoshiriki katika hadithi (Wamitila, 2002). Kwa mantiki hiyo, Nadharia ya Naratolojia imetuwezesha kubaini mtazamo wa kisiasa kupitia sauti ya nafsi ya pili kwa kuwa karibu na simulizi kwa sababu jambo analozungumza anahusika nalo na anataka kumshirikisha msomaji kupitia sauti ya nafsi ya pili (Bal, 1997).

Kwa ujumla, sauti ya nafsi ya pili inaonesha mtazamo wa kisiasa kwa namna mbili: mosi, kupitia msimulizi anaposhirikisha wasomaji wake au anapozungumza na hadhira yake, na pili, kupitia mazungumzo baina ya wahusika. Hata hivyo, usimulizi wa nafsi ya pili hauna mawanda mapana kama ilivyo nafsi ya kwanza na nafsi ya tatu. Aidha, Nadharia ya Naratolojia imetuwezesha kuchambua usimulizi wa nafsi ya pili ulivyotumika kuibua mtazamo wa kisiasa kama vile masuala ya uongozi mbaya, usaliti, damokrasia, ubinafsishaji na kukosekana kwa uzalendo wa viongozi kwa wanajamii.

### 5.3 Sauti ya Nafsi ya Tatu

Sauti ya nafsi ya tatu hutumia kiambishi “a” au neno “yeye” katika umoja na kiambishi “m” au neno “ninyi” katika wingi. Kwa mujibu wa Mbijima (2018), kuna aina anuwai za sauti za nafsi ya tatu ambazo ni sauti ya usimulizi maizi, tinde na horomo.

#### 5.3.1 Sauti ya Usimulizi Maizi

Sauti ya msimulizi maizi ni mbinu ya usimulizi inayotumika katika kazi za ubunifu ikiwamo hadithi fupi. Katika usimulizi maizi, msimulizi anakuwa huru sana na anajua kila kitu katika hadithi. Kupitia sauti ya msimulizi huyu tunaweza kujua mawazo ya wahusika wengine. Msimulizi maizi huingia katika akili za wahusika na kufunua mawazo yao. Pia, huweza kueleza kile ambacho mhusika anakumbuka na kuonesha msimamo wake kuhusu masuala mbalimbali (Mohochi, 2000; Sisakht, 2014; Burundi, Makuthuria na Matundura, 2017; Mbijima, 2018; Mahenge, 2019; Chapanga, 2021). Kwa hiyo, msimulizi maizi ana uhuru wa kuamua yapi asimulie na huweza kuingia katika akili za wahusika na kutueleza yaliyomo. Sauti ya usimulizi maizi hutokea pale ambapo msimulizi anakuwa na sifa za kiungu za kujua siri za wahusika wote na anajua mambo yote katika hadithi. Pia, msimulizi huyo ana uwezo wa kujua hisia na ndoto za wahusika (Mbijima, 2018).

Sauti ya usimulizi maizi inajitokeza katika hadithi fupi ya *Msomi Aliyebinafsishwa*, pale ambapo msimulizi anasimulia kwa kutumia sauti ya usimulizi maizi na kuibua mtazamo wa kisiasa kama tuonavyo hapa chini:

> Nyagichuro **aliendelea kujiuliza** maswali yaso kichwa wala mkia “hawajui kuwa baada ya kusaini mkataba wa uwekezaji ndipo nilipewa zawadi ya ufadhili? Hawaoni kuwa wamepunguziwa mzigo sana? Sasa mwekezaji amekubali kunifadhili kusomea digrii ya PhD kuhusu sera ya Ubinafsishaji. Kwa hakika Wanakong’amu wakiniletea mchezo nitawabinafsisha bila wao wenyewe kujua! Nitabinafsisha ardhi yao! Nitawabinafsisha mabinti zao! Zaidi nitabinafsisha wake zao! Hapo ndipo watakapojua kuwa mimi ndiye msomi aliyebinafsishwa kwa manufaa ya kulisaidia taifa” Nyagichuro **alipayukapayuka** pasipo mpangilio wowote. (uk. 8)

Kutokana na dondoo hilo, tunaona sauti ya kupitia sauti ya msimulizi maizi akisimulia mawazo ya mhusika Nyagichuro kuhusu ubinafsishaji. Mhusika Nyagichuro anaona ubinafsishaji una umuhimu mkubwa kutokana na kufadhiliwa masomo ya PhD bila kujali hali za wananchi wanaobinafsishwa. Kwa hiyo, mtazamo alionao Nyagichuro ni wa kufanya ubinafsishaji kwa ajili ya masilahi yake na siyo masilahi ya wananchi. Katika sauti ya usimulizi maizi, msimulizi ana uwezo wa kusimulia mawazo ya mhusika kwa sababu anafahamu kila kitu kuhusu

wahusika na matukio katika usimulizi. Kwa hiyo, msimulizi anakuwa na uhuru wa kueleza fikra za mhusika yeyote kadiri aonavyo yeye.

Pia, katika hadithi ya *Msomi Aliyebinafsishwa* sauti ya usimulizi maizi inajitokeza pale ambapo msimulizi anasimulia kuhusu ujio wa kiongozi wa ngazi ya juu kitaifa ambaye ni Nyagichuro pamoja na msafara wake. Katika kusimulia tukio hili, msimulizi anaingia katika fikra na akili za wazee na kuona jambo wanalowaza kwa wakati ule. Hebu tuangalie maelezo ya msimulizi katika dondoo lifuatalo:

> Gari la polisi liliwasili asubuhi na mapema kijijini Kong'amu. Wanasungusungu **waliwalazimisha** wanakijiji wote kujipanga barabarani ili wampokee Nyagichuro. **Nyagichuro alikuwa** kiongozi wa kwanza kitaifa kutembelea kijiji hicho tangu uhuru upatikane. Wanafunzi wa shule za msingi na sekondari walikuwa wameandaa nyimbo, michezo, mashairi na kila aina ya burudani ili kumburudisha Nyagichuro… **wanakijiji wa Kong'amu walianza kuhofu**. **Walihofu** juu ya ule msafara! **Hawajawahi** kuona msafara kama ule tangu nchi ipate uhuru. Wazee wa zamani **walifikiria** ni mzungu amerudi tena (uk.10)

Kutokana na dondoo hilo, tunaona msimulizi akitumia sauti ya nafsi ya tatu kusimulia kuhusu ujio wa viongozi katika kijiji cha Kong'amu na namna ambavyo wanatukuzwa kutokana na nyadhifa walizonao na wala siyo kwa uwajibikaji wao. Kwa hiyo, kupitia nukuu hiyo, tunaona pia mtazamo wa wazee wa zamani kupitia msimulizi ambaye amepata uhuru wa kuangalia mawazo yao katika akili zao. Hali hii inathibitisha kuwa sauti ya usimulizi maizi ina uwezo wa kiungu wa kuingia katika akili za watu na kuona mawazo yao na mtazamo wao. Katika hali hiyo ndipo tunaona mtazamo wa kisiasa unaoonesha kutokuwajibika kwa viongozi katika nafasi zao.

Vilevile, sauti ya usimulizi maizi inajitokeza anaposimulia ndoto ya Nyagichuro ambaye akiwa usingizini, anaota mama yake anataka kumuua kwa kumwingiza kwenye tanuri la moto. Hii inamaanisha kuwa msimulizi ana uhuru uliopitiliza hadi kujua ndoto za mhusika na mambo anayowaza katika ndoto, jambo ambalo katika usimulizi wa aina nyingine haliwezekani. Msimulizi anasema:

> **Nyagichuro yupo usingizini… anaota anapiga kelele**. "Mama usinikamate. Mama usiniue. Mama nimewatetea wanyonge. Mama nimewaletea maendeleo wanyonge. Waulize Wanakong'amu nimeamua kijibinafsisha mwenyewe ili niwaletee wanakijiji maendeleo" (uk.11).

Katika dondoo hilo, tunasikia sauti ya mhusika Nyagichuro ambaye ni kiongozi wa kisiasa, kupitia ndoto ambayo inasimuliwa na msimulizi. Katika ndoto hiyo

Nyagichuro anaeleza kuwa ameleta maendeleo na kuwatetea wanyonge kupitia ubinafsishaji. Katika maelezo yake tunapata mtazamo wa udanganyifu na usaliti wa viongozi kwa wananchi wanaowaongoza. Kupitia nukuu hiyo, tunaweza kuona kuwa msimulizi anafahamu mawazo na hisia za wahusika wengine, anajua kila kitu kuhusu wao kama asemavyo Madumulla (2009) kuwa msimulizi maizi hujipa uhuru mkubwa kabisa wa kuingia katika fikra na hisia za wahusika wake kadiri atakavyo na kuwapatia habari na mielekeo kadiri anavyotaka.

Vilevile, katika hadithi ya *Shingo ya Mbunge* sauti ya usimulizi maizi wa nafsi ya tatu inajitokeza pale ambapo msimulizi anasimulia na kuingia katika akili ya mbunge. Katika dondoo lifuatalo msimulizi anasema:

> **Lazima Mbunge alitambua** kosa alilokuwa amefanya. Alimkazia macho; akanigeukia kisha akamwangalia Levina. “Ahh, bila shaka… Nakujua wewe ni…” ***alisema huku akijaribu kuliopoa jina lake kwenye mapori ya akili yake.*** Ili kuifunika fedheha yake, alipenyeza kicheko cha kujilazimisha (uk. 56).

Katika dondoo hili tunapata mtazamo wa uongozi mbaya kupitia sauti ya mbunge, Dan Magraba. Hapa tunaona namna mbunge alivyokuwa hawajali wala hawajibiki kwa watu wake. Kupitia sauti ya usimulizi, msimulizi anataka tusikie sauti inayoeleza usahaulifu wa mbunge kwa wananchi wake. Katika hali hiyo, msimulizi, kutokana na sifa za kiungu, anaingia katika akili ya mbunge na kuona namna anavyotafuta majina katika kumbukumbu zake. Hali hii inadhihirisha kuwa mbunge alikuwa hawajibiki kwa wananchi wake. Hapa pia tunaona namna sauti ya usimulizi maizi ilivyo na uhuru mkubwa wa kuingia katika akili za wahusika na kufahamu mawazo yao katika hadithi hii.

### 5.3.2 Sauti ya Usimulizi Horomo

Sauti ya usimulizi horomo ni ile inayopatikana katika nafsi ya tatu ambapo msimulizi husimulia kisha huacha wahusika wazungumze wenyewe bila kuwaingilia wanayozungumza (Mbijima, 2018). Hii inamaanisha kuwa katika sauti ya usimulizi horomo, msimulizi huwapa nafasi wahusika wazungumze wenyewe bila kuwaingilia. Hivyo, msimulizi hana uhuru wa kuwaingilia mazungumzo yao.

Katika hadithi fupi ya *Msomi Aliyebinafsishwa*, sauti ya usimulizi horomo inajitokeza kuonesha mtazamo wa kisiasa. Wahusika wanazungumza namna viongozi wa kisiasa na wasomi wanavyokubali uwekezaji na ubinafsishaji ambao umeleta madhara kwa wanakijiji wa Kong’amu. Msimulizi anawapa nafasi mama, Nyagichuro na Entakana kutoa mitazamo yao bila kuwaingilia wala kufafanua walichozungumza. Hilo linajibainisha katika lifuatalo:

> "**Kila kitu kimebinafsishwa! Machimbo ya dhahabu ya Goga… Mbuga za wanyama ya Gwitonga… Msitu mkubwa wa Masanga… Balaa limefikia kijiji chetu!" Entakana alilalamika** kuhusu hali ya uwekezaji. "Wabunge wetu wanaona! **Wanaubariki uwekezaji! Wanabariki wizi wa dhahabu! Wanabariki wizi wa magogo! Wanabariki wizi wa wanyama na pembe zao! Wanafurahia wizi wa ndege wetu wazuri! Wasomi wetu wamekaa kimya! Wasomi wetu wanashangilia maovu tunayotendewa" Nyagento alilalamika.** Hii ilikuwa ni siku ambayo Entakana alirudi likizo nyingine kijijini (uk. 9).

Kupitia dondoo hilo, tunaona sauti ya nafsi ya tatu ikieleza kuhusu ubinafsishaji unaofanywa na viongozi wa kisiasa. Hata hivyo, katika sauti horomo, msimulizi hukaa kando kwa muda ili kuonesha mtazamo wa wahusika hao. Pia, msimulizi huchagua matukio ya kuwaachia wazungumze ili kufikisha ujumbe sehemu husika. Sisakht (2014) anasema kuwa katika aina hii ya usimulizi, wahusika ndio husimulia jambo ambapo wahusika hao hutoa mitazamo yao. Naye Mbijima (2018) anaongezea kuwa wahusika hao huchagua matukio kwa makusudi huku wakikazia na kusisitiza jambo ambalo litamwacha msomaji njiapanda. Kwa hiyo, ni dhahiri kuwa katika sauti ya nafsi ya tatu horomo, msimulizi huchagua matukio ambayo huwaacha wahusika wazungumze bila kuwaingilia. Pia, msimulizi hutoa nafasi kwa wahusika ili kuonesha sauti tofautitofauti kama tunavyoona kwenye nukuu. Lengo ni kuonesha namna wahusika wanavyoangalia matukio kwa mitazamo tofautitofauti.

### 5.3.3 Sauti ya Usimulizi Tinde

Sauti ya usimulizi tinde ni aina mojawapo ya sauti ya nafsi ya tatu ambayo hutumika kuonesha sauti ya hisi, mawazo na mambo yanayojulikana na mhusika mmoja au wahusika wachache miongoni mwa waliopo katika hadithi (Mbijima, 2018; Chapanga, 2021). Sauti ya usimulizi tinde husimulia jambo kulingana na hisia za mhusika au namna wahusika wengine wanavyomwona. Kwa mfano, katika hadithi ya *Msomi Aliyebinafsishwa,* sauti ya usimulizi imetumika kusimulia hisia za Nyagichuro akiwa kijiji cha Kong'amu kwamba kutokana na wadhifa wake, hawezi kushirikiana na wanakijiji. Dondoo lifuatalo linaonesha aina hii ya sauti:

> Nyagichuro huyoo! Ameshuka jukwaani. Anaelekea kwenye gari. Ameziba pua ili asivute harufu chafu ya Kong'amu. Wanakijiji wengi wanajitahidi wamshike mkono, wapi! Polisi hawataki kiongozi wa ngazi ya juu kitaifa ashikwe mkono na mlala hoi! (uk. 11).

Katika dondoo hlo tunaona namna sauti ya usimulizi tinde ilivyotumika katika kusimulia hadithi kulingana na hisia za Nyagichuro kwa wananchi, kiongozi huyo

anaonekana kuziba pua na kukataa kushikwa mkono na wanakijiji wa Kong'amu. Pia, katika *Shingo ya Mbunge* kuna sauti ya usimulizi tinde inayojitokeza kupitia msimulizi ambaye ni mwanakijiji, anayesimulia kuhusu ahadi ya mbunge na mambo aliyoyafanya. Msimulizi anasema:

> Katika siku mia moja zangu kama Mbunge nitahakikisha kuwa pamejengwa majosho manne na kwamba yana dawa za kutosha. Aliahidi. Hayo majosho hayakujengwa. Machache yaliyokuwako hayakuzipata dawa zilizohitajika; mojawapo liliharibiwa katika siku hizo alizosema. **Lakini alihakikisha amefanya jambo mojawapo amejenga jumba kubwa ambalo halikuwa na kifani katika eneo bunge nzima**. (uk. 51).

Hapa sauti ya usimulizi tinde imetumika kumsimulia mhusika mbunge ambaye hakutimiza ahadi zake baada ya kupata uongozi. Hivyo, kupitia nukuu hiyo, tunaona sauti ya usimulizi tinde inayotoa mtazamo wa uongozi mbaya katika nchi ya dunia ya tatu kwa kuwa wengi wanashindwa kutekeleza ahadi wanazoweka kipindi cha kampeni badala yake viongozi wengi wanajilimbikizia mali. Kwa hiyo, msimulizi anaeleza mawazo ya wananchi kuhusiana na mbunge kushindwa kutimiza ahadi zake kwa wananchi wake. Hivyo, msimuizi tinde husimulia mawazo au mambo yanayojulikana na mhusika ambaye ni miongoni mwa waliomo katika hadithi (Mbijima, 2018). Hii inamaanisha kuwa sauti ya usimulizi tinde hujikita kwa mhusika mmojawapo katika simulizi ili kuonesha namna anavyoangalia jambo husika. Hili linajitokeza dhahiri katika nukuu hiyo na kupitia sauti ya msimulizi tinde tumepata mtazamo wa kisiasa hasa wa kutowajibika kwa viongozi, kujilimbikizia mali na usaliti wa viongozi kwa wananchi.

## 6.0 Hitimisho

Kwa ujumla, uchambuzi wa sauti za usimulizi katika kazi za fasihi ni muhimu kuchunguzwa ili kutambua sauti zimebeba mtazamo gani katika kazi husika. Mara nyingi sauti hizo zinaweza kuonesha mitazamo mbalimbali kwa kuzingatia nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Katika makala haya tumejikita katika kuelezea sauti za usimulizi zilivyotumika kubaini mtazamo wa kisiasa. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Naratolojia, tumebaini mitazamo mbalimbali ya kisiasa iliyojitokeza katika hadithi fupi teule. Baadhi ya mitazamo ya kisiasa iliyojitokeza ni ubinafsishaji, uongozi mbaya, masuala ya demokrasia, matabaka, usaliti wa viongozi, ufisadi, kujilimbikizia mali, kukosekana kwa uzalendo na uhujumu uchumi. Aidha, makala haya yameibua masuala mbalimbali ya kisiasa ambayo ndani yake kuna masuala ya kijamii na kiuchumi.

**Marejeleo**

Bal, M. (1997) *Introduction to the Theory of Narrative*. London: University of Toronto Press.

Kuhn, M. (2009) Film Narratology: Who Tells? Who Shows? Who Focalizes? Narrative Mediation in Self-Reflexive Fiction Films. Katika P. Hühn, W. Schmid . na J. Schönert (Wah.) *Narratology: Point of View, Perspective and Focalization*: *Modeling Mediation in Narrative* (Juz. 17). Berlin: De Gruyter. Inapatikana katika https://doi.org/10.1515/9783110218916. Ilisomwa tarehe 20/04/2023

Burundi, R. N., Matundura, E. na Makuthuna, M. (2017) "Usimulizi katika Utenzi wa Swifa ya Nguvu Mali". *Kioo cha Lugha*, Juz. 12: 73-85.

Chapanga J. D. (2021) *Ujitokezaji wa Mtazamo wa Kisiasa katika Hadithi Fupi Shingo ya Mbunge na Msomi Aliyebinafsishwa*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Evans, O. B. (2005) *Uhakiki wa Usimulizi katika Riwaya ya Walenisi*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Nairobi, Nairobi.

Ferguson, S. (1978) "Defining the Short Story: Impressionism and Forms". *Modern Fiction Studies*. Juz. 28: 13-24.

Fludernik, M. (2009) *An introduction to Narratology*. USA: Routledge.

Genette, G. (1980) *Narrative Discourse: An Essay in Method.* New York. Colnell University Press.

Keen, S. (2003) *Narrative Form.* Washington: Pulgrave Macmillan.

Mahenge, E. G. (2019) *Uumbaji wa Ualbino katika Fasihi ya Kiswahili: Uchambuzi wa Kazi Teule*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Mbijima, R. J. (2018) "Usimulizi katika Nagona na Mzingile: Aina na Athari zake kwa Msomaji" Katika S. O. Mchepange na M. Samwel (Wah.) *Fasihi Lugha na Utamaduni wa Kiswahili na Kiafrika.* Dar es Salaam: TATAKI. kur. 132-158.

Msokile, M. (1992) *Misingi ya Hadithi Fupi.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Madumulla, J. S. (2009) *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi.* Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.

Mohochi, E. S. (2000) "Usimulizi wa Nyongo Mkalia Ini". *Nordic Journal of African Studies*. Juz. 9(2): 49- 59. Inapatikana katika https://www.njas.fi/njas/article/view/620/443. Ilisomwa tarehe 10 Aprili 42021.

Monolov, G. V. (2007) *Elements of Narrative Discourse in Selected Short Stories of Ernest Hemingway*. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha South Florida, Florida.

Prince, G. (1982) *Narratology*: *The Form and Functioning of Narrative*. New York: Mouton Publishers.

Rasley, A. (2008) *The Power of Point of View*. Canada: Writer's Digest Books Publishers.

Rimmon-Kenan, S. (2002) *Narrative Fiction: Contemporary Poetics*. London: Routledge Taylor & Francis Group:

Sisakht, I. N. (2014) "Analysis of Narrative and Importance of Point of View in Novel". *International Journal of Science and Research*. Juz. 3(7): 181-183. Inapatikana katika https://www.ijsr.net/archive/v3i7/MDIwMTQ3NTc=.pdf Ilisomwa tarehe 10 Aprili 2021.

Wambui, J. (2018) *Usimulizi katika Riwaya ya Dharau ya Ini*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Wamitila, K. W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Dar es Salaam: Phoenix Publisher Ltd.

Wamitila, K. W. (2003) *Kamusi ya Istilahi za Fasihi*. Nairobi: Vide~ Muwa Publishers Limited.

Wamitila, K. W. (Mh.) (2007) *Shingo ya Mbunge na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Limited.

Wamitila, K. W. (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Limited.

Yirsaw, L. (2016) "A Comperative Study on Selected Short Stories of Leo Tolstoy and Edgar Allan Poe". *World Journal of English Language,* Juz. 6: 3-24. Inapatikana katika https://doi.org/10.5430/wjel.v6n3p24. Ilisomwa tarehe 20 Machi 2023.